Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Fedha














# HALI YA UCHUMI WA TAIFA 2025

Toleo la Mwananchi

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA 2025

## Toleo la Mwananchi

Wizara ya Fedha
Mji wa Serikali - Mtumba
Mtaa wa Hazina, 40468 Dododma



> "Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya uchumi kupitia uwekezaji mkubwa katika miradi ya kimkakati, huduma za kijamii na sekta za uzalishaji. Hatua hizi zimechangia kuongeza fursa za kiuchumi, kuimarisha ustawi wa wananchi na kuongeza ushindani wa uchumi wa Taifa. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kusisitiza maendeleo yenye tija kwa wananchi kupitia utekelezaji wa miradi inayochochea ajira, mapato na ushiriki mpana wa wananchi katika shughuli za maendeleo."

Waziri wa Fedha

**Mhe Balozi Khamis Mussa Omar**



Ni muhimu kwa wananchi kuwa na uelewa wa hali ya uchumi wa nchi kwa kuwa maendeleo ya uchumi yanagusa maisha ya kila siku ya jamii kupitia ajira, bei za bidhaa na huduma, uwekezaji pamoja na upatikanaji wa huduma za kijamii. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeandaa Taarifa ya Hali ya Uchumi Toleo la Mwananchi kama muhtasari wa taarifa kuu ya uchumi, ili kuwezesha wananchi kupata taarifa muhimu za maendeleo ya uchumi wa Tanzania.

Katibu Mkuu

**Dkt. Natu E. Mwamba**,

# Yaliyomo

**Muhtasari wa Takwimu** XII

**1. Ukuaji wa Uchumi** 1
- 1.1 Uchumi wa Dunia 1
- 1.2. Mfumuko wa Bei wa Dunia 3
- 1.3. Mfumuko wa Bei Kusini mwa Jangwa la Sahara 4
- 1.4. Uchumi wa Taifa 5
- 1.5. Mfumuko wa Bei wa Taifa 7

**2. Sekta ya Fedha** 8
- 2.1. Mikopo kwa Sekta Binafsi 8
- 2.2. Viwango vya Riba 8
- 2.3. Thamani ya Shilingi na Ujazi wa Fedha 9
- 2.4. Huduma za Benki na Mawakala wa Benki 9

**3. Sekta ya Nje** 10
- 3.1. Biashara ya Bidhaa 10
- 3.2. Biashara ya Huduma 11
- 3.3. Mizania ya Malipo na Nchi za Nje 11

**4. Rasilimali Watu** 13
- 4.1. Idadi ya Watu 13
- 4.2. Idadi ya Watu Kimkoa 13
- 4.3. Idadi ya watu kwa jinsi na Umri Tanzania 14
- 4.4. Nguvu Kazi na Ajira 14

**5. Fedha za Serikali** 17
- 5.1. Mapato ya Serikali 17
- 5.2. Mwenendo wa Matumizi 18

**6. Kilimo** 21
- 6.1. Mazao 21
- 6.2. Upatikanaji wa Pembejeo 22
- 6.3. Ufugaji 22
- 6.4. Uvuvi 24

**7. Viwanda na Biashara** 25
- 7.1. Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani 25
- 7.2. Usajili wa Viwanda na Biashara 26
- 7.3. Udhibiti Ubora wa Viwango na Vipimo 26
- 7.4. Usawa wa Ushindani na Udhibiti wa Bidhaa Bandia 27

**8. Madini** 29
- 8.1. Leseni za Shughuli za Madini 29
- 8.2. Vibali vya Uuzaji wa Madini 30
- 8.3. Madini 30

**9. Nishati** 31
- 9.1. Uwezo wa Uzalishaji wa Umeme 31
- 9.3. Gesi asilia 32

**10. Mawasiliano, Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo** 35
- 10.1. Mawasiliano 35
- 10.2. Habari 35
- 10.3. Maendeleo ya Sanaa 36

10.4. Maendeleo ya Michezo 36

**11. Ujenzi 37**

11.1. Mtandao wa Barabara 37

11.2. Usajili wa Makandarasi 38

11.3. Usajili wa Wahandisi 38

**12. Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo 39**

12.1. Usafiri 39

12.2. Abiria 40

12.2. Shehena Zilizohudumiwa 41

**13. Elimu 45**

13.1. Elimu ya Msingi 45

13.2. Elimu ya Sekondari 46

13.3. Elimu ya Ufundi Stadi-VETA 47

13.4. Elimu ya Juu 47

**14. Afya 48**

14.1. Vituo vya Kutolea Huduma za Afya 48

14.2. Udhibiti wa Kifua Kikuu 50

14.3. Udhibiti wa Malaria 50

14.4. Afya kwa Watoto 50

**15. Maji 51**

15.1. Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji 51

15.2. Upatikanaji wa Maji 51

**16. Maliasili na Utalii 55**

16.1. Utalii 55

16.2. Hifadhi za Taifa 56

**17. Uendelezaji wa Sekta Binafsi 57**

17.1. Usajili wa Miradi ya Uwekezaji 57

17.2. Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje 57

**18. Masuala Mtambuka 59**

18.1. Mazingira 59

18.2. Usalama wa Raia 59

18.3. Usajili, Ufilisi na Udhamini 59

**19. Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa 63**

19.1. Dhana na Umuhimu wa Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa 63

# Muhtasari wa Takwimu, Mwaka 2025

## Uchumi Jumla

**5.9%**
Ukuaji wa Pato la Taifa nchini

**3.4%**
Ukuaji wa Pato Duniani

**3.3%**
Mfumuko wa bei nchini

**4.1%**
Mfumuko wa bei duniani

**-2.8%**
Mikopo chechefu

**23.6%**
Mikopo kwa sekta binafsi

## Fedha za Serikali
(hadi Machi 2026)


Mapato ya Ndani
**30.8**
Shilingi Trilioni

Ridhaa ya matumizi
**35.4**
Shilingi Trilioni

Matumizi ya Maendeleo
**12.4**
Shilingi Trilioni

## Sekta za Uzalishaji

Ukuaji wa Uzalishaji wa baadhi ya Bidhaa Viwandani





**1.7%**
Ongezeko la thamani ya Uzalishaji wa bidhaa viwandani

**10.6%**
Ongezeko la uzalishaji dhahabu

**6.6%**
Ongezeko la umeme uliouzwa

## Miundombinu Wezeshi

### Hali ya mtandao wa barabara






**9.5%**
Ongezeko la abiria waliosafiri kwa njia ya anga

**34.1%**
Ongezeko la uwezo wa uzalishaji wa umeme

## Sekta Nyingine

**11.8%**
Ongezeko la kadi za simu

**12.1%**
Ongezeko la uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje


**0.4%**
Ongezeko la Uwekezaji wa Mojakwa moja kutoka nje

**6.1%**
Ukuaji wa Miradi iliyosajilliwa na TISEZA

**-51.4%**
Hati za talaka

## Suala Maalumu

### Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi Baada ya Maboresho ya Mwaka wa Kizio



# Uchumi Jumla

**Sehemu hii inahusisha mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa nchi mbalimbali, ikiwemo Tanzania, mfumuko wa bei, sekta zinazochangia katika ukuaji wa uchumi, pamoja na viashiria mbalimbali vya uchumi jumla.**

Uchumi jumla hujumuisha uchambuzi wa sera mbalimbali za kiuchumi, hususan sera za fedha na sera za bajeti, pamoja na athari na matokeo yake katika uchumi, ikiwemo ustawi wa wananchi, uwekezaji, matumizi, uzalishaji na utulivu wa bei. Aidha, uchambuzi wa masuala ya Uchumi husaidia kupanga mikakati ya maendeleo na matumizi bora ya rasilimali za nchi.





# 1. Ukuaji wa Uchumi

Uchumi uliendelea kuimarika kwa kuonesha ukuaji thabiti uliotokana na kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji na utekelezaji wa sera za kiuchumi zinazolenga uthabiti. Mfumuko wa bei uliendelea kubaki katika viwango vinavyokubalika.

## 1.1 Uchumi wa Dunia

**3.4%**

Ukuaji wa Uchumi wa dunia kwa mwaka 2025 kama ilivyokuwa mwaka 2024. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji kulikotokana na uwekezaji katika teknolojia ikiwemo matumizi ya akili unde pamoja na hatua zilizochukuliwa na nchi mbalimbali katika kukabiliana na mabadiliko ya sera za biashara.


**Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi Duniani Mwaka 2025**







**Chanzo:** Shirika la Fedha la kimatifa-WEO toleo la Aprili 2026

**Kielelezo Na 1.2: Wastani wa Ukuaji wa Uchumi wa Kikanda (Asilimia)**




**Chanzo:** Shirika la Fedha la kimatifa-WEO toleo la Aprili 2026






## 1.2. Mfumuko wa Bei wa Dunia


**4.1%**

Kiwango cha mfumuko wa bei wa dunia kwa mwaka 2025 ambacho kimepungua ikilinganishwa na asilimia 5.8 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuimarika kwa bei za bidhaa na huduma duniani kulitokana na utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kupunguza ongezeko la ukwasi, kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan mafuta na mbolea.



**2.7%**

Kiwango cha mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.9 mwaka 2024.



**13.5%**

Kiwango cha mfumuko wa bei kwa nchi za Ulaya zinazoibukia na zinazoendelea kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 17.2 mwaka 2024.




### 1.3. Mfumuko wa Bei Kusini mwa Jangwa la Sahara

**12.5%**

Mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikuwa wastani wa asilimia 12.5 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 20.7 mwaka 2024. Ongezeko la mfumuko wa bei lilitokana na sababu mbalimbali ikiwemo athari za kushuka kwa thamani ya fedha pamoja na uzalishaji usioridhisha katika shughuli za kilimo.

**Kielelezo Na 1.3: Wastani wa Mwenendo wa Mfumuko wa Bei (Asilimia)**




**Chanzo:** Shirika la Fedha la kimatifa-WEO toleo la Aprili 2026


## 1.4. Uchumi wa Taifa



**5.9%**

Ukuaji wa Pato halisi la Taifa mwaka 2025 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.6 mwaka 2024.


**Kielelezo Na. 1.4: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi Mwaka 2022-2025 (Asilimia)**




Sababu za Ukuaji wa Uchumi kwa mwaka 2025 ni pamoja na:

- Utekelezaji wa miradi ya kimkakati, hususan miundombinu ya nishati, maji, usafirishaji na huduma za jamii;
- Kuendelea kuimarika kwa sekta ya fedha, ikiwemo kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi;
- Kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji hususan kilimo, viwanda na uchimbaji wa madini na mawe;

**Kielelezo Na.1.5: Ukuaji wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi Mwaka 2025 (Asilimia)**






**15.7%**

Shughuli ya fedha na bima iliendelea kuongoza kwa kuwa na ukuaji mkubwa kuliko shughuli nyingine.



Shughuli za uzalishaji umeme zilifuatia kwa kuwa na ukuaji wa asilimia 11.8 pamoja na shughuli za uchimbaji madini na mawe asilimia 9.4.

**Kielelezo Na.1.6: Mchango wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi katika Pato la Taifa Mwaka 2025 (Asilimia)**





**24.3%**

Shughuli za kilimo ziliendelea kuongoza kwa kuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa ikifuatiwa na ujenzi asilimia 11.9 na uchimbaji madini na mawe asilimia 10.3

Shughuli za kilimo; fedha na bima; usafirishaji; madini; na ujenzi zilikuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa.



**Kielelezo Na.1.7: Mchango wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi katika Ukuaji wa Mwaka 2025 (Asilimia)**




## 1.5. Mfumuko wa Bei wa Taifa

**3.3%**

Kiwango cha mfumuko wa Bei kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2024.Ongezeko hilo lilitokana na kupanda kwa bei za baadhi ya vyakula, ikiwemo mahindi, mchele na ulezi.

**Kielelezo Na. 1.7. Mwenendo wa Mfumuko wa Bei kwa Baadhi ya Makundi**




Kiwango hicho kilikuwa ndani ya lengo la nchi la muda wa kati la asilimia 3.0 hadi 5.0.

**2.2%**

Kiwango cha wastani wa mfumuko wa bei za msingi kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2024.



**6.4%**

Kiwango cha mfumuko bei wa kwa kundi la chakula na vinywaji baridi mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.1 mwaka 2024.

**4.3%**

Mfumuko wa bei kwa kundi la nishati, mafuta na ankara za maji kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 9.3 mwaka 2024



# 2. Sekta ya Fedha

Sekta ya fedha nchini iliendelea kuwa imara, ikichochewa na ongezeko la amana, mikopo kwa sekta binafsi, na kuongezeka kwa huduma za mawakala wa benki. Aidha, kiwango cha mikopo chechefu kilipungua ikiashiria kuimarika kwa usimamizi wa mikopo na sekta ya fedha kwa ujumla.


### 2.1. Mikopo kwa Sekta Binafsi



**23.6%**

Ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi na kufikia shilingi bilioni 44,603.1 mwaka 2025 kutoka shilingi bilioni 36,097.4 mwaka 2024

**Kielelezo Na. 2.1: Mchango wa Mikopo Iliyotolewa na Benki za Biashara katika baadhi ya Shughuli za Kiuchumi (Asilimia)**




### 2.2. Viwango vya Riba

**9.58%**

Wastani wa riba za amana za mwaka mmoja mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 9.17 mwaka 2024.



**15.69%**

Wastani wa riba za mikopo ya mwaka mmoja mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 15.82 mwaka 2024

### 2.3. Thamani ya Shilingi na Ujazi wa Fedha

**2.3%**

Ongezeko la thamani ya shilingi katika mwaka 2025 ambapo dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,549.8 ikilinganishwa na shilingi 2,610.5 kwa dola moja ya Marekani mwaka 2024.




**29.6%**

Ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2 ) na kufikia shilingi bilioni 48,143.2 katika kipindi kilichoishia Desemba 2025.

### 2.4. Huduma za Benki na Mawakala wa Benki





**42**

Idadi ya benki nchini mwaka 2025 iliendelea kama ilivyokuwa mwaka 2024.

**29.1%**

Ongezeko la mawakala wa benki na kufikia mawakala 187,692 mwaka 2025 kutoka mawakala 145,430 mwaka 2024.



# 3. Sekta ya Nje

Sekta ya nje iliendelea kuimarika ikichochewa na kuongezeka kwa mauzo nje ya nchi, hususan bidhaa zisizo asilia. Aidha, urari wa malipo yote nje ya nchi uliendelea kuimarika kutokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma, hususan utalii.


## 3.1. Biashara ya Bidhaa



**12.5%**

Ongezeko la thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi na kufikia dola za Marekani milioni 10,262.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 9,121.6 mwaka 2024.


**Kielelezo Na. 3.1: Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa, Mwaka 2022-2025**





**4.2%**

Ongezeko la uagizaji wa bidhaa kutoka nje na kufikia dola za Marekani milioni 14,787.7 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 14,195.6 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji pamoja na bidhaa za matumizi ya kawaida.


**Kielelezo Na. 3.2: Mchanganuo wa Thamani ya Bidhaa Zilizouzwa Nje, Mwaka 2025**



**Kielelezo Na. 3.3: Mchanganuo wa Thamani ya Bidhaa Zisizoasili Zilizouzwa Nje Mwaka 2025**




**Kielelezo Na. 3.4: Mchanganuo wa Thamani ya Bidhaa zilizoagizwa kutoka Nje Mwaka 2025**





## 3.2. Biashara ya Huduma




**4.5%**

Ziada ya urari wa biashara ya huduma iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 4,235.7 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 4,051.7 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii na huduma za usafirishaji.

**Kielelezo Na. 3.5: Mwenendo wa Biashara ya Huduma Mwaka 2022-2025**




## 3.3. Mizania ya Malipo na Nchi za Nje

Urari wa Malipo yote

**968.9**

**Dola za Marekani milioni**

Ziada ya urari wa malipo yote ya nje kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 70.1 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma.

## Urari wa Biashara ya Bidhaa na Huduma

**289.1**


**Dola za Marekani milioni**

Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa na huduma kwa mwaka 2025 iikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,022.3 mwaka 2024, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 71.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ziada ya urari wa biashara ya huduma pamoja na kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa.

## Akiba ya Fedha za Kigeni

**6,329**

Dola za Marekani milioni



hadi Desemba 2025, kiasi kilichotosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.9.



# 4. Rasilimali Watu


Idadi ya watu nchini imeendelea kuongezeka kwa kasi, hali inayochochea ongezeko la mahitaji ya huduma za kijamii na kiuchumi. Sambamba na hilo, ukuaji wa miji, hususan katika miji mikuu, umeendelea kuimarika kutokana na uhamiaji wa watu unaochochewa na fursa za kiuchumi.

### 4.1. Idadi ya Watu

**2.8%**

Ongezeko la mwaka la makadirio ya idadi ya watu Tanzania kwa mwaka 2025 na kufikia 68,153,004 ikilinganishwa na watu 66,278,276 mwaka 2024. Aidha, wanawake walikadiriwa kuwa 34,732,602, sawa na asilimia 51.0 ya watu wote na wanaume walikuwa 33,420,402 (asilimia 49.0). Makadirio ya mwaka 2025 ni maoteo ya mwenendo wa matokeo ya Sensa ya Mwaka 2022 kwa kutumia mbinu ya kipeo

Makadirio ya Idadi ya watu kwa Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na mchango wake katika asilimia ya makadirio ya Jumla idadi ya watu Tanzania.






### 4.2. Idadi ya Watu Kimkoa

**8.9%**

Mchango wa idadi ya watu katika mkoa wa Dar es Salaam kwa idadi ya watu wote Tanzania Bara.



Mwaka 2025, mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu wapatao 5,874,418, ikifuatiwa na mkoa wa Mwanza uliokuwa na watu 4,116,854.

Idadi kubwa ya watu katika mkoa wa Dar es Salaam ilitokana na upatikanaji wa fursa mbalimbali za kiuchumi na huduma muhimu za kijamii zilizowavutia watu kuhamia kutoka mikoa mingine.

**47.2%**

Mchango wa mkoa wa Mjini Magharibi kwa jumla ya watu wote Tanzania Zanzibar.

**1.4 %**


Mkoa Njombe ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu, wapatao 956,702.

### 4.3. Idadi ya watu kwa jinsi na Umri Tanzania


**52.7%**

Asilimia ya Kundi la umri wa miaka 15-64 (nguvu kazi) liliongoza kuwa na mchango kumbwa katika idadi ya watu.

**Kielelezo Na. 4.1: Idadi ya Watu Tanzania Bara kwa Umri na Jinsia Mwaka 2025**




Sehemu kubwa ya watu walikuwa na umri wa miaka 15 - 34 ambao walichangia asilimia 33.9 ya idadi ya watu wote.



Watu wenye umri tegemezi ambao ni umri chini ya miaka 15 na umri wa miaka 65 na zaidi walikuwa 31,218,715, sawa na asilimia 47.3 ya watu wote.



### 4.4. Nguvu Kazi na Ajira

**3,990,458**

Jumla ya ajira rasmi kwa mujibu wa Utafiti wa Ajira na Mapato katika sekta rasmi mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 9.8 ikilinganishwa na 3,635,755 mwaka 2022/23.

**34.4%**

Mchango wa mkoa wa Dar es Salaam ambao uliongoza kwa idadi ya waajiriwa wote katika ajira rasmi mwaka 2023/24.

# Fedha za Serikali

## Sehemu hii inaangazia utekelezaji wa bajeti ya Serikali inayohusisha uchambuzi wa mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali

Fedha za Serikali hukusanywa kutoka vyanzo vya ndani na nje na hutumika kwa ajili ya kugharamia utoaji wa huduma kwa wananchi, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Serikali. Aidha, uchambuzi wa masuala ya Fedha za Serikali husaidia kufahamu uwezo wa Serikali kugharamia vipaumbele vya kitaifa na kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za umma



# 5. Fedha za Serikali

Serikali iliendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kusimamia matumizi ya fedha za umma ili kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, ikiwemo miradi ya kimkakati na huduma za jamii.


### 5.1. Mapato ya Serikali

**103.3%**


Ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ikilinganishwa na lengo la kipindi hicho.




**Kielelezo Na. 5.1: Mchanganuo wa Mapato ya Ndani kwa Kipindi cha Julai 2025-Machi 2026**




**Kielelezo Na. 5.2: Mchanganuo wa Misaada na Mikopo , Julai 2025-Machi 2026**



### 5.2. Mwenendo wa Matumizi




**Ridhaa ya matumizi ya maendeleo iliyotolewa ilijumuisha ugharamiaji wa miradi ya miundombinu wezeshi na huduma za jamii**


**103.3%**

Ridhaa ya matumizi iliyotolewa katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ikilinganishwa na lengo la kipindi hicho.

**Kielelezo Na. 5.3: Mchanganuo wa Matumizi bila Malipo ya Mtaji wa Deni la Serikali Katika Kipindi cha Julai 2025 - Machi 2026**




**Kielelezo Na. 5.4: Mchanganuo wa Malipo ya Deni la Serikali katika Kipindi cha Julai 2025-Machi 2026**



IV

# Sekta za Uzalishaji

**Sekta za uzalishaji zinaangazia mwenendo wa shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi; uzalishaji wa bidhaa viwandani na biashara; uchimbaji na uuzaji wa madini; pamoja na uzalishaji na upatikanaji wa nishati nchini.**



Sekta za uzalishaji hujumuisha shughuli zinazotumia rasilimali na pembejeo mbalimbali kuzalisha chakula, malighafi, bidhaa na nishati kwa ajili ya matumizi na biashara. Aidha, uchambuzi wa sekta hizi husaidia kufahamu uwezo wa nchi katika uzalishaji, usalama wa chakula, maendeleo ya viwanda, mapato ya fedha za kigeni, upatikanaji wa nishati na mchango wake katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi.



# 6. Kilimo

Sekta ya kilimo iliendelea kuimarika ambapo uzalishaji wa mazao uliongezeka kutokana na kuimarika kwa huduma za ugani, matumizi ya teknolojia, upatikanaji wa pembejeo bora na mvua za kutosha. Hii iliwezesha kuongezeka kwa ziada ya chakula pamoja na kuimarika kwa usalama wa chakula.

## 6.1. Mazao

### Mazao ya Chakula




**130.1%**

Kiwango cha utoshelevu wa chakula nchini kinachotokana na mazao makuu ya chakula mwaka 2025. Aidha, kiwango cha utoshelevu wa chakula kinachojumuisha mazao ya chakula, mifugo na samaki kulingana na dhana ya mizania ya chakula (Food Balance Sheet) ulikuwa asilimia 112.

**4.3%**

Ongezeko la uzalishaji wa mazao makuu ya chakula kufikia tani 23,783,128 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 22,803,316 mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 6.1. Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Chakula Mwaka 2022-2025**





### Mazao ya Biashara

**13.4%**

Ongezeko la uzalishaji wa mazao asilia ya biashara kufikia tani 1,687,105 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 1,487,364 mwaka 2024.



**Kielelezo Na. 6.2. Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Biashara Mwaka 2022-2025**





Ongezeko la uzalishaji wa mazao kwa ujumla lilitokana na kuimarika kwa huduma za ugani, kilimo cha umwagiliaji, utafiti, uwepo wa hali nzuri ya hewa.



**Mazao ya Bustani**

**30.2%**

Ongezeko la uzalishaji wa mazao ya bustani unaojumuisha maua, matunda, viungo na mboga na kufikia tani 9,782,338 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 7,513,502 mwaka 2024.

**6.2. Upatikanaji wa Pembejeo**

**Mbegu Bora**

**72,031** tani


upatikanaji wa mbegu bora mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 72,032 mwaka 2024.

**Mbolea**

**9.1%**

Ongezeko la upatikanaji wa mbolea kufikia tani 1,323,798 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na tani 1,213,780 mwaka 2023/24.

**Kielelezo Na.6.3. Mwenendo wa Uzalishaji na Matumizi ya Mbolea Mwaka 2021/22–2024/25**




**6.3. Ufugaji**


**Uzalishaji wa Mifugo**

**3.4%**

Ongezeko la idadi ya ng'ombe nchini na kufikia ng'ombe 40,569,621 mwaka 2025 ikilinganishwa na ng'ombe 39,241,375 mwaka 2024



**Kielelezo Na. 6.4. Mwenendo wa Idadi ya Mifugo Mwaka 2024 - 2025**




## Uzalishaji wa Mazao ya Mifugo

**4.4%**

Ongezeko la uzalishaji wa nyama na kufikia tani 1,100,489.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 1,054,114.0 mwaka 2024.




**5.2%**

ongezeko la uzalishaji wa maziwa mwaka 2025 na kufikia lita 4,218,529.2 ikilinganishwa lita 4,009,985.3 mwaka 2024.


**10.9%**

Ongezeko la uzalishaji wa mayai na kufikia 7,878,320 mwaka 2025 ikilinganishwa na mayai 7,105,908 mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 6.5. Uzalishaji wa Nyama Mwaka 2024-2025**




**Kielelezo Na. 6.6. Uzalishaji wa Mayai mwaka 2022-2025**




### 6.4. Uvuvi

#### Uvunaji wa Samaki


Mwaka 2025, tani 519,650.5 za samaki zenye thamani ya shilingi bilioni 5,375.78 zilivunwa ikilinganishwa na tani 522,788.3 zenye thamani ya shilingi bilioni 4,352.73 zilizovunwa mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 6.7. Mwenendo wa Uvunaji wa Samaki mwaka 2022-2025**




Mwaka 2025, samaki hai wa mapambo 259,876 na tani 45,053.4 za mazao ya uvuvi zenye thamani ya shilingi bilioni 648.91 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na samaki hai wa mapambo 173,377 na tani 59,746.4 za mazao ya uvuvi zenye thamani ya shilingi bilioni 677.55 zilizouzwa mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 6.8. Mchanganuo wa Aina ya Uvunaji Samaki kwa Mwaka 2025**







# 7. Viwanda na Biashara

Sekta ya viwanda na biashara iliendelea kuimarika kutokana na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Maendeleo hayo yaliambatana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa viwandani, ajira, usajili wa biashara na viwanda pamoja na kuimarika kwa huduma za uendelezaji wa wajasiriamali na teknolojia.


### 7.1. Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani

**0.7%**

Ongezeko la thamani ya bidhaa zilizozalishwa viwandani kufikia shilingi bilioni 27,923.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 27,725.7 mwaka 2024.




**Kielelezo Na. 7.1. Ukuaji wa Uzalishaji wa Baadhi ya Bidhaa za Viwandani Mwaka 2025**




**1.7%**

Ongezeko la gharama za uzalishaji bidhaa viwandani kufikia wastani wa shilingi bilioni 12,056.4 mwaka 2025 ikilinganishwa shilingi bilioni 12,039.2 mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 7.2. Matumizi ya Saruji Nchini (000' Tani), mwaka 2022-2025**






### 7.2. Usajili wa Viwanda na Biashara

**10.4%**

Ongezeko la kampuni zilizosajiliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni - BRELA na kufikia kampuni 18,489 mwaka 2025 ikilinganishwa na kampuni 16,748 zilizosajiliwa mwaka 2024.

**6.2%**

Ongezeko la majina ya biashara yaliyosajiliwa na BRELA na kufikia 32,670 mwaka 2025 ikilinganishwa na majina 30,753 mwaka 2024

**16.2%**

Ongezeko la leseni za biashara daraja "A" zilitolewa na BRELA na kufikia 23,653 mwaka 2025 ikilinganishwa na leseni 20,364 zilizotolewa mwaka 2024.

**33.7%**

Ongezeko la leseni za viwanda zilizotolewa na BRELA kufikia 496 mwaka 2025 ikilinganishwa na leseni 371 mwaka 2024.

Ongezeko la usajili na utoaji wa leseni lilitokana na kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya ufanyaji biashara, ikiwemo matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika utoaji wa leseni pamoja na mafunzo kwa maafisa biashara na elimu kwa umma.

### 7.3. Udhibiti Ubora wa Viwango na Vipimo

**15.7%**

Ongezeko la sampuli zilizopimwa na kufikia 44,809 mwaka 2025 ikilinganishwa na sampuli 38,724 zilizopimwa mwaka 2024.



Ongezeko la sampuli zilizopimwa na TBS lilitokana na na kuimarishwa kwa ukaguzi na ufuatiliaji katika masoko pamoja na uwekezaji katika vifaa vya kisasa vya maabara.

## 7.4. Usawa wa Ushindani na Udhibiti wa Bidhaa Bandia

**-3.6%**

Kupungua kwa maombi ya muungano wa kampuni yaliyoidhinishwa na Tume ya Ushindani – FCC na kufikia maombi 54 mwaka 2025 ikilinganishwa maombi 56 mwaka 2024. Maombi hayo yalitoka katika sekta za kilimo, uzalishaji viwandani, fedha, afya, mawasiliano, madini, biashara na nishati.

**6,411**

Makasha yaliyokaguliwa na FCC mwaka 2025 ikilinganishwa na makasha 6,357 yaliyokaguliwa mwaka 2024. Kati ya hayo, makasha 471 yalibainika kuwa na bidhaa bandia.





# 8. Madini

Shughuli za madini ziliendelea kuimarika kutokana na ongezeko la uzalishaji na mauzo nje ya nchi. Aidha, shughuli za madini ziliendelea kuwa chanzo muhimu cha mapato ya fedha za kigeni na kuchochea shughuli za kiuchumi, ikiwemo ukuaji wa viwanda vinavyotumia malighafi za madini.

#### 8.1. Leseni za Shughuli za Madini

**24.6%**

Ongezeko la leseni za utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, usafishaji na biashara ya madini zilizotolewa na kufikia leseni 14,958 mwaka 2025 ikilinganishwa na leseni 12,009 mwaka 2024.

Hii ilitokana na kuboreshwa kwa mfumo wa utoaji leseni wa Trimble landfolio na kutolewa kwa mafunzo kwa watumiaji wa Mfumo huo pamoja na kuongezeka kwa vitendea kazi.



## 8.2. Vibali vya Uuzaji wa Madini

**19.5%**

Ongezeko la thamani ya vibali vya kuuza madini nje ya nchi kufikia dola za Marekani milioni 4,991.13 ikilinganishwa na thamani ya dola za Marekani milioni 4,176.18 vilivyotolewa mwaka 2024.

## 8.3. Madini




### Dhahabu

**10.6%**

Ongezeko la uzalishaji wa madini ya dhahabu kufikia kilogramu 68,225.38 mwaka 2025 ikilinganishwa na kilogramu 61,680.81 zilizozalishwa mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 8.1: Mwenendo wa Uzalishaji na Kiasi cha Dhahabu Kilichopata Vibali vya Kuuzwa Nje, Mwaka 2022 - 2025**




### Almasi

**9.3%**

Ongezeko la uzalishaji wa madini ya almasi kufikia karati 407,840.00 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 63.55 ikilinganishwa na karati 373,252.76 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 59.24 zilizozalishwa mwaka 2024

### Vito vya Thamani

**-36.4%**

Upungufu wa uzalishaji madini ya vito ghafi kufikia kilogramu 29,447,271 mwaka 2025 ikilinganishwa na kilogramu 46,299,069 zilizozalishwa mwaka 2024

### Tanzanite

**73.8%**

Ongezeko la uzalishaji wa madini ya tanzanite ghafi na magonga kufikia kilogramu 144,308.48 ikilinganishwa na kilogramu 83,014.66 mwaka 2024

### Makaa ya Mawe

**-0.6%**

Upungufu wa makaa ya mawe yaliyozalishwa na kufikia tani 3,879,960.85 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 3,904,542.69 zilizozalishwa mwaka 2024.

V

# Miundombinu Wezeshi

Miundombinu wezeshi inaangazia maendeleo katika sekta za nishati, ujenzi, uchukuzi na uhifadhi mizigo ikiwemo hatua zinazoendelea kuchukuliwa kuimarisha miundombinu hiyo muhimu kwa ajili ya kuvutia uwekezaji na biashara nchini.

Miundombinu wezeshi inaweka mazingira bora kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kufanyika kwa ufanisi. Inahusisha uwekezaji katika sekta muhimu zinazorahisisha uzalishaji, usafirishaji wa bidhaa na huduma, biashara, pamoja na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.



# 9. Nishati


Sekta ya nishati iliendelea kuimarika kupitia uwekezaji katika miundombinu ya uzalishaji na usambazaji wa nishati ikiwemo umeme na gesi. Nishati ya kutosha na ya uhakika ni muhimu katika maendeleo ya viwanda na uendeshaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii nchini.

### 9.1. Uwezo wa Uzalishaji wa Umeme

**34.1%**

Ongezeko la uwezo wa uzalishaji wa umeme na kufikia megawati 4,093.74 mwaka 2025 ikilinganishwa na megawati 3,052.46 mwaka 2024.


**Kielelezo Na 9.1: Ukuaji wa Uwezo wa Uzalishaji wa Umeme, Mwaka 2023-2025**




Mwaka 2025, umeme uliozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali ulikuwa saa za megawati (MWh) 13,887,330 ikilinganishwa na saa za megawati 11,958,840 zilizozalishwa mwaka 2024.



**Kielelezo Na. 9.2: Mchanganuo wa Umeme Uliozalishwa Mwaka 2025**







Mitambo ya umeme ya nguvu ya maji iliongoza kwa kuchangia kiasi cha asilimia 63.84 cha umeme uliozalishwa katika Gridi ya Taifa kutokana na kuendelea kwa uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere

**6.6%**

Ongezeko la umeme uliouzwa kwa watumiaji mbalimbali na kufikia saa za megawati (MWh) 9,713,000 mwaka 2025 ikilinganishwa na saa za megawati (MWh) 9,114,700 zilizouzwa mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 9.3: Mwendendo wa Umeme Uliouzwa, Mwaka 2022-2025 (MWh '000)**




**Kielelezo Na. 9.4: Mchanganuo Umeme Uliouzwa kwa Watumiaji Mbalimbali Mwaka 2022 - 2025 (MWh '000')**





### 9.3. Gesi asilia


**-11.0%**

Upungufu wa uzalishaji wa gesi asilia futi za ujazo milioni 61,905.84 mwaka 2025.

**Kielelezo Na. 9.5: Mwenendo wa Uzalishaji wa Gesi Asilia, Mwaka 2022-2025**




**Kielelezo Na. 9.6: Mwenendo wa Bei ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa katika Soko la Ndani Mwaka 2025 (Shilingi/Lita)**



# 10. Ujenzi

Shughuli za ujenzi ikiwemo miundombinu ya barabara ziliendelea kuimarika nchini hivyo kuimarisha shughuli za usafiri na usafirishaji na kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi.


**10.1. Mtandao wa Barabara**

**181,883.59** km


Mtandao wa barabara nchini mwaka 2025 ikilinganishwa na kilometa 181,864.81 mwaka 2024.




**Kielelezo Na. 10.1: Usimamizi wa Mtandao wa Barabara Mwaka 2025.**



**Kielelezo Na.10.2: Mchanganuo wa Hali ya Mtandao wa Barabara Kuu na za Mikoa Mwaka 2025**



### 10.1.Usajili wa Makandarasi

**1,643**


Idadi ya makandarasi waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi - CRB mwaka 2025 ikilinganishwa na makandarasi 1,812 waliosajiliwa mwaka 2024.

### 10.2. Usajili wa Wahandisi

**3,501**

Idadi ya wahandisi waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi - ERB mwaka 2025 ikilinganishwa na wahandisi 3,636 waliosajiliwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 3.7.

**Kielelezo Na.10.3: Mchanganuo wa Wahandisi Waliosajiliwa na Bodi ya Wahandisi kwa mwaka 2025**



# 11. Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo

Mwaka 2025, sekta ya uchukuzi na uhifadhi mizigo iliendelea kuonesha maendeleo chanya, hususan katika utoaji wa leseni za usafiri wa barabara, ukuaji wa huduma za usafiri wa anga na kuimarika kwa shughuli za bandari.

### 11.1. Usafiri


**Usafiri wa barabarani**

**14.5%**

Ongezeko la leseni zilizotolewa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini – LATRA kwa vyombo vya moto vilivyosajiliwa kutoa huduma ya usafirishaji kibiashara ikilinganishwa na leseni 329,112 zilizotolewa mwaka 2024.




**Kielelezo Na. 11.1: Mwenendo wa Utoaji wa Leseni za Usafirishaji Mwaka 2022-2025**





**Ajali za barabarani**

**-11.8%**


Upungufu wa ajali katika vyombo vya usafirishaji wa abiria na mizigo ulitokana na kuendelea na kaguzi za mara kwa mara barabarani, matumizi ya mfumo wa kufuatilia mwendendo wa mabasi ya masafa marefu



**Kielelezo Na. 11.2: Mchanganuo wa Ajali Mwaka 2025**



**Kielelezo Na. 11.3: Mchanganuo wa Ajali Mwaka 2022-2025**




### 11.2. Abiria

**Usafiri wa Reli**

**131.7%**

Ongezeko la abiria walisafirishwa na Shirika la Reli Tanzania kupitia reli ya kisasa kwa kiwango cha kimataifa - SGR kufikia abiria 3,294,934 mwaka 2025 ikilinganishwa na abiria 1,422,116 waliosafirishwa mwaka 2024.




**Usafiri wa Anga**

**9.5%**

Ongezeko la abiria waliosafiri kwa njia ya anga kufikia abiria 8,111,107 mwaka 2025 ikilinganishwa na abiria 7,404,408 waliosafiri mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa miruko ya ndege, kuanza safari mpya kwa baadhi ya mashirika ya ndege.



**Kielelezo Na. 11.4: Mchanganuo wa Abiria Mwaka 2025**





**2.8%**

Ongezeko la mizigo iliyosafirishwa kupitia njia ya anga na kufikia tani 44,076.0 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 42,884.5 zilizosafirishwa mwaka 2024 kufuatia kuimarika kwa biashara ya usafiri wa anga pamoja na ongezeko la idadi ya watalii nchini.



### 11.3. Shehena Zilizohudumiwa




**27.7%**


Ongezeko shehena zilizohudumiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania - TPA na kufikia tani milioni 35.7 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani milioni 28.1 zilizohudumiwa mwaka 2024.

**29.8%**

Ongezeko shehena zilizohudumiwa katika Bandari Kuu za mwambao na kufikia milioni 31.8 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani milioni 24.5 zilizohudumiwa mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 11.5: Mchanganuo wa Shehena Zilizohudumiwa kwa Bandari Mwaka 2025**





# Huduma za jamii

**Huduma za jamii zinaangazia maendeleo katika utoaji wa huduma za elimu, afya na maji, ikiwemo upatikanaji wa miundombinu na huduma katika ngazi mbalimbali, pamoja na hatua zinazochukuliwa kuboresha maisha ya wananchi.**

Huduma za jamii hujumuisha huduma muhimu zinazochangia maendeleo ya rasilimali watu na ustawi wa jamii, hususan elimu, afya pamoja na upatikanaji wa maji safi na salama. Aidha, uchambuzi wa huduma hizi husaidia kufahamu upatikanc na ubora wa huduma kwa wananchi, maendeleo ya kijamii na mchango wake katika kujenga jamii yenye afya, maarifa uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shug za maendeleo.





# 12. Elimu

Sekta ya elimu, mafunzo ya ufundi na teknolojia iliendelea kuimarika kutokana na upanuzi wa miundombinu, ongezeko la udahili na maboresho ya elimu katika ngazi mbalimbali.

## 12.1. Elimu ya Msingi


### Idadi ya Shule

**1.7%**

ongezeko la idadi shule za msingi kufikia 20,889 mwaka 2025 kutoka shule 20,533 mwaka 2024.




**Kielelezo Na. 12.1: Mwenendo wa Idadi Usajili wa Vilabu vya Michezo, Mwaka 2022-2025**




Ongezeko la idadi ya shule za msingi lilitokana na juhudi za Serikali kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na shule ya msingi



**Kielelezo Na. 12.2: Mwenendo wa Idadi Shule za Msingi za Serikali na Zisizo za Serikali, Mwaka 2021-2025**





### Idadi ya Wanafunzi


**0.3%**

Ongezeko la idadi ya wanafunzi katika shule ya elimu ya msingi ilikuwa 11,428,424 mwaka 2025 ikilinganishwa na wanafunzi 11,391,185 mwaka 2024

**Kielelezo Na. 12.3: Mchanganuo Wanafunzi katika Shule ya Elimu ya msingi , Mwaka 2025**




**Kielelezo Na. 12.4: Mwenendo wa Idadi ya Watahiniwa na waliofaulu Darasa la Saba, Mwaka 2020-2025**




### Uwiano wa Mwalimu kwa Wanafunzi shule za Elimu ya Msingi za Serikali na zisizo za Serikali Mwaka 2025

**1:49**

Uwiano uliendelea kuboreshwa mwaka 2025 ikilinganishwa na uwiano wa 1:50 mwaka 2024.




## 12.2. Elimu ya Sekondari

### Idadi ya Shule


**3.5%**

Ongezeko la idadi shule za sekondari kufikia kufikia 6,488 ikilinganishwa na shule 6,269 mwaka 2024. Hii ilitokana na jitihada za Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kuongeza idadi ya madarasa na shule mpya za sekondari kukabiliana na idadi kubwa ya wanafunzi waliohitimu darasa la saba na kujiunga na kidato cha kwanza.

**Kielelezo Na. 12.5: Mwenendo wa Idadi ya Shule za Sekondari ('000), Mwaka 2022-2025**





**Kielelezo Na. 12.6: Mwenendo wa Idadi ya Shule za Sekondari, Mwaka 2022-2025**




**3.4%**

3.4% Ongezeko la Idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari kidato cha kwanza hadi cha sita kufikia 3,425,822 mwaka 2025 ikilinganishwa na wanafunzi 3,314,198 mwaka 2024.


**Kielelezo Na. 12.7: Mgawanyo wa Wanafunzi za Sekondari Kidato cha I-VI Mwaka 2025**





**Kielelezo Na. 12.8: Mgawanyo wa Wanafunzi kwa Jinsia Katika Shule za Sekondari Kidato cha I-VI Mwaka 2025**




**Kielelezo Na. 12.9: Mwenendo wa Idadi ya Watahiniwa na Ufaulu Kidato cha Nne, Mwaka 2022-2025**




**Kielelezo Na. 12.10: Mwenendo wa Idadi ya Watahiniwa na Ufaulu Kidato cha Sita, Mwaka 2021-2024**




## 12.3. Elimu ya Ufundi Stadi-VET

**11.2%**

Ongezeko la idadi ya wanafunzi katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi – VETAkufikia wanafunzi 30,785 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wanafunzi 27,676 mwaka 2023/24.


## 12.4. Elimu ya Juu

**Idadi ya Wanafunzi**

**7.9%**

Ongezeko la wanafunzi katika taasisi za elimu ya juu nchini na kufikia wanafunzi 361,257 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wanafunzi 334,854 mwaka 2023/24. Hii ilitokana na upatikanaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu pamoja na kuongezeka kwa programu zinazotolewa.

**Kielelezo Na. 12.11: Mwenendo wa Idadi wa Elimu ya Juu 2024/25**



# 13. Afya


Sekta ya afya iliendelea kuimarika kutokana na upanuzi wa huduma, uboreshaji wa miundombinu na kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za matibabu kwa wananchi.

## 13.1. Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

**6.5%**

Ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya na kufikia vituo 13,683 mwaka 2025 kutoka vituo vya kutole huduma za afya 12,846 mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 13.1: Mchanganuo wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya kwa Umiliki Mwaka 2025**






**7.4%**

Ongezeko la wagonjwa walipatiwa huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi na kufikia 4,134 mwaka 2025 ikilinganishwa na wagonjwa 3,849 mwaka 2024.



## Huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi zilizotolewa zilijumuisha

- Upandikizaji wa figo
- Upandikizaji wa uroto
- Uwekaji wa puto kwa ajili ya kupunguza uzito
- upasuaji wa moyo kwa kutumia mtambo maalum
- Upandikizaji wa vifaa vya usikivu kwa watoto
- Upandikizaji wa nyonga bandia
- Upasuaji wa magoti kwa njia ya matundu
- Huduma za upandikizaji mimba.

### 13.2. Udhibiti wa Kifua Kikuu


**5.2%**

Kuongezeka kwa wagonjwa wa kifua kikuu na kufikia wagonjwa 80,639 mwaka 2025 ikilinganishwa na wagonjwa 76,684 mwaka 2024.

**22.3%**


Ongezeko la idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya matibabu ya kifua kikuu sugu na kufikia 373 mwaka 2025 kutoka vituo 305 mwaka 2024

### 13.3. Udhibiti wa Malaria



Mwaka 2025, vipimo 28,206,100 vya malaria na vichupa 1,926,133 vya dawa ya sindano ya kutibu malaria kali vilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya afya.

**Kielelezo Na. 13.2: Idadi ya Wagonjwa Waliolazwa katika Vituo vya kutolea Huduma za Afya, Mwaka 2024-2025**





### 13.4. Afya kwa Watoto




**10.4%**

Ongezeko la idadi ya watoto waliozaliwa katika vituo vya kutolea huduma za afya na kufikia watoto 2,449,812 mwaka 2025 kutoka watoto 2,219,417 mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 13.3: Watoto wa Chini ya Mwaka Mmoja Waliopata Chanjo Mwaka 2025**



# 14. Maji

Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha usimamizi endelevu na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini. Aidha, Serikali iliendelea na uchimbaji wa visima pamoja na ujenzi wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi.

## 14.1. Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

Mwaka 2025, kiwango cha rasilimali za maji kinachofaa kwa matumizi kiliendelea kuwa wastani wa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka kama kilivyokuwa mwaka 2024.


**1,907.5**

**Mita za Ujazo**

Kiasi cha maji kwa mtu ambacho ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa.


## 14.2. Upatikanaji wa Maji

**Kielelezo Na. 14.1: Mwenendo wa Wastani wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji Mijini na Vijijini, Mwaka 2022-2025**






**Kielelezo Na. 14.2: Wateja walioonganishwa na Mtandao wa Majitaka, Mwaka 2022-2025**



# Sekta Nyingine

**Sekta nyingine zinaonesha mwenendo wa shughuli za maliasili na utalii, uendelezaji wa sekta binafsi pamoja na masuala mtambuka yanayohusu mazingira, usalama wa raia, usajili, ufilisi na udhamini nchini.**

Sekta nyingine zinajumuisha shughuli na huduma zinazochangia kuvutia watalii na uwekezaji, kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi, kuhifadhi mazingira na kuendeleza ustawi wa jamii. Aidha, uchambuzi wa sekta hizi husaidia kufahamu mchango wa utalii katika mapato na fedha za kigeni, mwenendo wa uwekezaji na ajira, pamoja na hatua za kuimarisha mazingira, usalama wa raia na huduma za kijamii





# 15. Mawasiliano, Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

Sekta za mawasiliano, habari, utamaduni, sanaa na michezo ziliendelea kuonesha mafanikio mbalimbali ikiwemo upanuzi wa huduma za mawasiliano, ongezeko la matumizi ya intaneti na maendeleo ya utamaduni na sanaa. Hata hivyo, baadhi ya huduma kama posta zilipungua kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia za kidijitali.

## 15.1. Mawasiliano

### Huduma za Posta

**-23.5%**

Upungufu wa barua zilizosafirishwa na Shirika la Posta Tanzania na kufikia barua 604,152 ndani ya nchi mwaka 2025 ikilinganishwa na barua 789,299 zilizosafirishwa mwaka 2024. Hii ilitokana na kuendelea kukua kwa matumizi ya njia za kidijitali katika mawasiliano ikiwemo barua pepe na simu za mkononi.



### Huduma za Simu

**23.1%**

Ongezeko la kadi za simu za kiganjani na kufikia 106,823,601 mwaka 2025 kutoka kadi 86,769,161 mwaka 2024.

### Huduma za Intaneti

**21.0%**


Ongezeko la kadi za simu zinazotumia intaneti na kufikia milioni 58.1 mwaka 2025 kutoka kadi za simu milioni 48.0 mwaka 2024



**39.3%**

Ongezeko la matumizi ya Intaneti nchini kufikia milioni 2,731 mwaka 2025.

## 15.2. Habari




**10.8%**

Ongezeko la vituo vya redio vilivyosajiliwa na kupewa leseni

na kufikia 277 mwaka 2025 kutoka vituo vya redio 250 mwaka 2024. Ongezeko la usajili na utoaji leseni lilichangiwa na kukua kwa hitaji la kupashana habari na kupungua kwa gharama ya leseni kwa baadhi ya huduma kufuatia mabadiliko ya kanuni.

**Kielelezo Na. 15.1: Mchanganuo wa Usajili wa Vyombo vya Habari, Mwaka 2022 - 2025**





## 15.3. Maendeleo ya Sanaa

**11.9%**

Ongezeko la wasanii binafsi waliosajiliwa na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kufikia 1,110 mwaka 2025 ikilinganishwa na wasanii 992 waliosajiliwa mwaka 2024.



**Kielelezo Na. 15.2: Mchanganuo wa Wasanii Binafsi Waliosajiliwa Mwaka 2025**




## 15.4. Maendeleo ya Michezo



**5.4%**

Ongezeko la usajili wa wadau wa michezo na kufikia wadau 329 mwaka 2025 ikilinganishwa na wadau 312 mwaka 2024.



# 16. Maliasili na Utalii

Sekta ya maliasili na utalii iliendelea kuchangia ukuaji wa uchumi kupitia ongezeko la watalii, mapato ya utalii na fedha za kigeni. Mafanikio hayo yalitokana na kuimarika kwa shughuli za utangazaji wa vivutio vya utalii na uboreshaji wa huduma za utalii nchini.

## 16.1. Utalii

**7.1%**


Ongezeko la watalii walioingia nchini kufikia 2,294,495 ikilinganishwa na watalii 2,141,895 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutangaza utalii kupitia programu maalum, balozi za Tanzania katika nchi mbalimbali, matamasha, mikutano na matukio mbalimbali, pamoja na utalii wa faru weusi na weupe.




**13.0%**

Ongezeko la mapato yatokanayo na watalii wa kimataifa kufikia dola za Marekani milioni 4,410.6 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,903.0 mwaka 2024

**Kielelezo Na. 16.1: Mwenendo wa Biashara ya Utalii Nchini, Mwaka 2021-2024**





**Kielelezo Na. 16.2: Mchanganuo wa Watalii Waliongia Nchini kwa Mae-neo Waliotembelea Mwaka 2024**






### 16.2. Hifadhi za Taifa

**Kielelezo Na. 16.3: Mchanganuo wa Watalii waliotembelea Hifadhi za Taifa 2025**




Mwaka 2025, Watalii 1,547,820 walitembelea Hifadhi za Taifa ikilinganishwa na watalii 2,010,239 mwaka 2024.



# 17. Uendelezaji wa Sekta Binafsi

Sekta binafsi iliendelea kuimarika kupitia ongezeko la uwekezaji, usajili wa miradi mipya na kuongezeka kwa mtaji kutoka ndani na nje ya nchi. Hali hiyo ilichangiwa na kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya biashara na uwekezaji.

### 17.1. Usajili wa Miradi ya Uwekezaji


**6.1%**

Ongezeko la miradi iliyosajiliwa na Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania - TISEZA mwaka 2025. Kati ya hiyo, miradi 297 ilikuwa ya wawekezaji wa ndani, miradi 475 ya wageni na miradi 184 ya ubia kati ya wawekezaji wa ndani na wageni.

**22.7%**

Ongezeko la thamani ya miradi iliyosajiliwa na kufikia dola za Marekani milioni 11,429.80 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 9,312.69 mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 17.1: Mchanganuo wa Miradi iliyosajiliwa Mwaka 2025**




### 17.2. Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje

**12.1%**

Ongezeko la uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje na kufikia dola za Marekani milioni 24,754.1 mwaka 2024 kutoka dola za Marekani milioni 22,074.4 mwaka 2023 kwa mujibu wa Taarifa ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2025.

**1,656.0**

**Dola za marekani milioni**

Thamani ya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,648.9 mwaka 2023.

**Kielelezo Na. 17.2: Mchanganuo wa Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje ya Nchi Mwaka 2024**



# 18. Masuala Mtambuka

Masuala mtambuka yaliendelea kupewa kipaumbele kupitia usimamizi wa mazingira, kuimarika kwa usalama wa raia pamoja na maboresho katika huduma za usajili na udhamini. Hatua hizo zilichangia kuimarisha ustawi wa jamii, uhifadhi wa mazingira na utoaji wa huduma kwa wananchi.

### 18.1. Mazingira

**-69.7%**

Upungufu wa miradi iliyopata hati za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na kufikia miradi 534 ikilinganishwa na miradi 1,764 mwaka 2024.

**24.2%**

Ongezeko la uwekezaji katika biashara ya Kaboni kufikia jumla ya kampuni 82 kutoka kampuni 66 mwaka 2024





### 18.2. Usalama wa Raia

**-6.0%**

Upungufu wa makosa makubwa ya jinai yaliyotolewa taarifa na wananchi na kufikia makosa 47,526 mwaka 2025 ikilinganishwa na makosa 50,574 yaliyotolewa taarifa mwaka 2024

**Kielelezo Na. 18.1: Mchanganuo wa Makosa Makubwa ya Jinai Mwaka 2024**





### 18.3. Usajili, Ufilisi na Udhamini


**-51.4%**

Upungufu wa hati za talaka zilizosajiliwa kufikia hati 762 mwaka 2025 ikilinganishwa na hati 1,569 zilizosajiliwa mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 18.2: Mwenendo wa Hati za Viapo vya Ndoa na Hati za Talaka, Mwaka 2021-2024**



**Kielelezo Na. 18.3: Idadi ya Usajili wa Hati Mbalimbali chini ya Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini - RITA kwa Mwaka 2025**



# Suala Maalum

**Suala maalumu linaangazia maboresho ya takwimu za Pato la Taifa, ikiwemo mabadiliko ya mwaka wa kizio, matumizi ya taarifa za karibuni na uhuishaji wa mfumo wa ukokotoaji ili kuakisi kwa usahihi zaidi mwenendo wa uchumi wa Tanzania.**

Maboresho ya takwimu za Pato la Taifa huzingatia mabadiliko katika uzalishaji, matumizi, uwekezaji, bei, biashara pamoja na kuibuka kwa shughuli mpya za kiuchumi. Aidha, uchambuzi wa suala hili husaidia kufahamu namna takwimu zilizoboreshwa zinavyotoa picha halisi zaidi ya ukubwa na ukuaji wa uchumi, na hivyo kuimarisha msingi wa upangaji wa sera na mipango ya maendeleo.





# 19. Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa

Maboresho ya takwimu za Pato la Taifa yalifanyika ili kuimarisha usahihi na ubora wa taarifa za ukuaji wa uchumi. Maboresho hayo yalihusisha matumizi ya taarifa za karibuni na kuzingatia mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia katika ukokotoaji wa Pato la Taifa.

## 19.1. Dhana na Umuhimu wa Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa



Maboresho ya takwimu za Pato la Taifa yanahusisha kubadilisha mwaka wa kizio uliopitwa na wakati na kutumia mwaka wa kizio wenye taarifa za karibuni. Maboresho hayo hufanyika kutokana na: Takwimu za mwaka wa kizio husika kupitwa na wakati; Uhitaji wa kujumuisha mabadiliko ya uzalishaji, matumizi, uwekezaji, bei ya bidhaa pamoja na taarifa mpya kutoka katika sensa na tafiti; Uzingatiaji wa matakwa mapya UNSNA na miongozo ya kuanisha shughuli za kiuchumi.

Lengo ni kuhakikisha ukokotoaji wa Pato la Taifa unaendana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia.


**Kielelezo Na. 19.1: Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa**

| Maboresho | Mwaka wa Kizio 2015 | Mwaka wa Kizio 2019 |
|---|---|---|
| 2015 | 94,349,316 | 93,591,198 |
| 2016 | 108,362,324 | 105,696,548 |
| 2017 | 118,742,133 | 116,596,419 |
| 2018 | 123,997,772 | 129,186,992 |
| 2019 | 134,540,194 | 139,135,212 |
| 2020 | 145,384,353 | 149,620,933 |
| 2021 | 156,167,137 | 161,468,405 |
| 2022 | 170,820,032 | 178,515,913 |
| 2023 | 186,753,685 | 192,868,267 |
| 2024 | 205,846,493 | 211,779,525 |
| 2025 | 228,510,423 | 234,104,003 |

# 13%

Ongezeko la thamani ya Pato halisi kwa mwaka 2019 na kufikia shilingi bilioni 139.14 kwa mwaka wa kizio 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 123.14 mwaka wa kizio 2015.

**Kielelezo Na. 19.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi Baada ya Maboresho**





Hali ya Uchumi wa Taifa 2025

**Toleo la Mwananchi**

Wizara y fedha
Mji wa Serikali - Mtumba
Mtaa wa Hazina
S.L.P 2802
Dodoma

http://www.mof.go.tz